

TANGAZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya **Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE)** na **Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA)**, mwaka **2025** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha usajili kwa Watahiniwa wa Kujitegemea kimeanza tarehe **01/01/2025** hadi **28/02/2025**. Ada ya usajili ni Shilingi **50,000/=** kwa **Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE)** na Shilingi **10,000/=** kwa **Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA)**. Aidha, watakoajisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01/03/2025** hadi **31/03/2025** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa ajili ya **Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE)** na Shilingi **15,000/=** kwa ajili ya **Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA)** ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Kabla ya kusajiliwa na Mkuu wa Kituo kwenye mtandao, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua namba rejea (**reference numbers**) zinazotolewa **bure** na kufanya malipo ya ada kupitia Benki kwa kutumia '**Control Number**'.
3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika kutengeneza '**Control Number**' na kujisajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania: www.necta.go.tz. Aidha, kwa watahiniwa ambao hawataweza kutumia mfumo huo wapige simu **0738785945** kwa msaada zaidi.
4. Waombaji wote wasisitizwa kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa mara baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na:

KATIBU MTENDAJI